Your complimentary use period has ended. Thank you for using PDF Complete.
Click Here to upgrade to Unlimited Pages and Expanded Features

BANK OF TANZANIA

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

***BoT yapongeza ugawaji misaada Gongo la Mboto***

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeipongeza serikali ya mkoa wa Dar es Salaam kwa kuweka utaratibu mzuri wa kupokea na kugawa misaada inayotolewa kwa ajili ya waathirika wa mabomu yaliyolipuka katika Kambi ya Jeshi ya Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam.

Naibu Gavana (Utawala na Udhibiti wa Ndani), Bw. Juma Reli, alitoa pongezi hizo Alhamisi wakati akitoa mkono wa pole kwa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Leonidas Gama, katika ofisi inayoshughulikia maafa hayo iliyoko Ukonga-Mombasa, jijini Dar es Salaam.

Alisema mahali penye maafa, wahalifu hupenda kutumia mwanya huo kujinufaisha na hivyo kuwakatisha tamaa watu wanaotoa misaada kwa ajili ya waathirika.

ñKuweka kumbukumbu za mahesabu vizuri, kuwa na ghala la kupokea misaada hiyo na kuruhusu wananchi kukagua mchakato mzima wa kupokea na kutoa misaada kwa walengwa ni hatua muhimu na chachu ya kuwavuta watu na taasisi zingine kuendelea kutoa misaada yao,ò alisema.



*Naibu Gavana (Utawala na Udhibiti wa Ndani),, Bw. Juma Reli (kushoto), akimkabidhi hundi ya sh. milioni 10 Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Leonidas Gama, kwa ajili ya waathirika wa mabomu Gongo la Mboto. Wanaoshuhudia ni Kaimu Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala, Bw. Richard Wambali, na Afisa Mwandamizi wa Benki Kuu,Bi. Resty Nkya.*

***Picha zote na Epimakus Mikuza (Aprili 14, 2011)***

Your complimentary use period has ended. Thank you for using PDF Complete.

Click Here to upgrade to Unlimited Pages and Expanded Features

milioni 10 kuchangia maafa hayo ya Februari 16, 2011 25, majeruhi wengi na uharibifu mkubwa wa nyumba na mali, zikiwemo nyumba 70 zilizobomolewa kabisa.

ñKwa niaba ya Gavana (Prof. Benno Ndulu), tumekuja kuwasilisha mchango wetu kufuatia maafa haya makubwa. Sisi kama taasisi ya umma tumeguswa tukaona tuchangie kuwafariji wenzetu,ò alisema Bw. Reli aliyefuatana na Kaimu Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala wa BoT, Bw. Richard Wambali.

Kwa niaba ya Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Gama, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Ilala, aliishukuru Benki Kuu kwa kuamua kushirikiana na jamii na akamuomba Naibu Gavana afikishe salamu za Mkoa kwa Gavana na wafanyakazi wote wa Benki Kuu.

ñMchango wenu tunauthamini sana; na mchango huu utawafikia walengwa,ò alisema Bw. Gama na kuongeza kuwa, ñtumejenga mfumo mzuri wa kusimamia misaada hii kuhakikisha inafika kwa walengwa.ò

Alisema kila mlengwa akipewa kifaa chochote anatia saini katika daftari maalum la watu wanaopokea misaada ambalo liko wazi kwa kila mwananchi kulikagua na kujihakikishia kuwa msaada wake umewafikia walengwa.

ñMtu yeyote na wakati wowote ana nafasi ya kuona mwenendo mzima wa misaadaé Misaada yenu tunaisimamia sana ili malengo yenu (kwa walengwa) yatimie,ò alisema.

Aidha, Kaimu Mkuu wa Mkoa huyo alieleza hatua mbalimbali zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na serikali kuwasaidia waathirika. Hatua hizo ni panoja na kuwazika waliokufa, matibabu, huduma za chakula na malazi, kujenga nyumba mpya na kuzikarabati zingine.

Baada ya hafla ya kukabidhi msaada, Naibu Gavana na ujumbe wake walitembelea na kujionea wenyewe baadhi ya nyumba zilizobomolewa na milipuko ya mabomu. Aidha, walifika katika shule ya sekondari ya Pugu ambako mkoa unatumia vyumba vinne vya madarasa kutunzia misaada mbalimbali inayotolewa kwa ajili ya tukio hilo la kusikitisha.

Mabomu yalilipuka katika ghala ya Kambi ya Jeshi la Wananchi ya Gongo la Mboto usiku wa Februari 16, 2011 na kusababisha maafa makubwa. Mpaka sasa waathirika wengi wa mabomu hayo wanaendelea kupatiwa misaada na serikali katika maeneo wanayoishi, huku wengine wakiwa bado wanaishi kwenye mahema.

PDF Complete
Your complimentary use period has ended. Thank you for using PDF Complete.
Click Here to upgrade to
Unlimited Pages and Expanded Features





***Picha za juu:*** *Maafisa wa Benki Kuu ya Tanzania wakiangalia nyumba Mama Abdul wa eneo la Malka kata ya Ukonga iliyopigwa na bomu. Wakazi wake wote walinusurika.*





*Naibu Gavana akiwa eneo la Mwembe Madafu akiangalia mabaki ya vyombo vya nyumba iliyobomolewa na bomu na kuua watu watano –mama na watoto wake wakati wakikimbia kutafuta usalama. Wenye nyumba walisalimika kwa kuwa walikwishakimbia mapema.* ***Kulia:*** *Naibu Gavana akizungumza kabla ya kukabidhi hundi kwa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.*





***Kushoto****: Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Leonidas Gama, akizungumza baada ya kupokea cheki kutoka kwa Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Juma Reli.* ***Kulia:*** *Bw. Herick Foya, afisa utumishi wa Manispaa ya Ilala, anayesimamia ghala la misaada kwa waathirika lilipo katika Shule ya Sekondari ya Pugu, akimwongoza Naibu Gavana na Kaimu Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala kuangalia misaada hiyo. Bw. Foya alisema wanajitahidi kugawa misaada hiyo kwa walengwa ili waweze kuyaacha madarasa manne na ofisi mbili za shule hiyo wanazozitumia. Alisema hivi sasa wanafunzi wa Kidato cha Tano wameanza kuripoti na hivyo kufanya madarasa hayo yahitajike. Bw. Foya alisema, waathirika wanapatiwa misaada mbalimbali kwa ajili ya kujikimu, lakini wanalalamikia ukosefu wa nishati. "Tatizo lao wanasema chakula mmetupa, tutapikia nini? Wanahitaji mkaa, gesi na pesa ili wayaendeshe maisha yao vizuri. Aidha, alisema wanalazimika kuwapa maturubai madogo yanayotolewa na UNHCR badala ya yale ya serikali – kama yanavyoonekana kwa mbali kutokana na maeneo ambayo waathirika hao wanakaa kuwa finyu.*

Your complimentary use period has ended. Thank you for using PDF Complete.
Click Here to upgrade to Unlimited Pages and Expanded Features



*Moja ya vyumba vya kutunzia misaada ya chakula.*

**Imetolewa na Idara ya Uhusiano na Itifaki**

Aprili 14, 2011